NIPASHE UK 9.

Majaliwa: Serikali inawathamini wafugaji

Na Mwandishi Wetu

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, amesema serikali inawathamini wafugaji na itaendelea kuboresha sekta yao.

Aliyasema hayo juzi wakati akiwasalimia wananchi waliojitokeza kumlaki kwenye kata ya Bukundi, Tarafa ya Nyaranje, wilayani Meatu, akiwa njiani kutoka Mkalama, Singida.

"Tunatambua na kuwathamini sana wafugaji kwa sababu tunajua mifugo ni fedha," alisema wakati akimwombea kura mgombea urais kwa tiketi ya CCM, Dk. John Magufuli, mgombea ubunge wa Jimbo la Meatu, Leah Komanya na mgombea udiwani wa kata ya Bukundi, James Sombi.

"Serikali yenu imedhamiria kuboresha sekta ya mifugo nchi nzima na ndiyo maana waziri mwenye dhamana ya mifugo, amekuwa anakutana na wafugaji nchi nzima, ili waeleze ni maeneo gani yanawapa kero."]

Alisema, serikali iliruhusu vijiji 920 kati ya 970 vilivyokuwa kwenye maeneo ya hifadhi virasimishwe, ili wananchi waendelee na ufugaji na kilimo.

Alisema, eneo la Bukundi lina wakazi wengi ambao asilimia 60 kati ya hao ni wafugaji. Amewaomba wagombea hao wakipita, warudi kwa wananchi na kutatua kero zao kwenye sekta ya mifugo.

Mapema, mgombea ubunge wa Jimbo la Kisesa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, alisema wakati serikali ya awamu ya tano inaingia madarakani, majosho 1,000 kati ya 2,400 yaliyokuwapo yalikuwa ni mabovu. "Chini ya uongozi wa rais wetu jemedari, Dk. Magufuli, majosho 600 yamekarabatiwa na tumejenga majosho mengine mapya 104. Yote yamepewa dawa ya ruzuku na wafugaji wanayatumia kuosha mifugo yao," alisema.

Scanned with CamScanner

WAFANYAKAZI wa Kiwanda cha Galaxy Food and Beverages Limited, wazalishaji wa [illegible] Kilimanjaro fresh wa mkoani Arusha, John Thomas na Jamila Juma, wakifungasha bidhaa tayari kwa kupelekwa sokoni (Picha na Shakila Nyerere).

Makosa ya Jinai katika mkoa huo.

UHURU UK 5

*Wafugaji, wauzaji maziwa 400 wanufaika na soko

Hai
NA SHAKILA NYERERE

VYAMA vya Ushirika vya Maziwa vya mkoani Kilimanjaro na Kiwanda cha Maziwa cha Kilimanjaro Fresh vimefanikiwa kuwanufaisha wafugaji na wauzaji maziwa zaidi ya 400 kwa kuwapatia uhakika wa soko la maziwa.

Wafugaji kila siku asubuhi na jioni wamekuwa wakikusanya maziwa kupeleka katika Kiwanda cha Kilimanjaro Fresh huku wengine wakiyapeleka katika vyama vya ushirika vilivyoingia ubia na kiwanda kwa ajili ya kupima maziwa kama yapo salama ili yakauzwe.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Meneja na mtaalamu wa maziwa kutoka Kilimanjaro Fresh, John Bagaka, alisema wameamua kuanzisha vituo vya kukusanya maziwa kwa

kushirikiana na vyama vya ushirika ili kupanua soko kwa wafugaji.

Bagaka alisema lengo ni kuona kila mfugaji anafuga kwa tija kutokana na soko ambalo wanalipata kupitia ushirikiano wa Kilimanjaro Fresh na Vyama vya Ushirika vya Maziwa.

"Kilimanjaro Fresh tumekuwa mfano wa kuigwa na viwanda vingine vya maziwa tunawajali wafugaji kwa kununua Maziwa yanayoletwa kiwandani hapo,"alisema Bagaka.

Aliongeza kuwa hatua hii ni mwanzo, lakini kiwanda hicho kinatarajia kuongeza kiwango cha ukusanyaji maziwa.

Bagaka alisema hivi sasa wanakusanya maziwa lita 10,000 lakini matarajio yao ni kukusanya lita 72,000 kwa siku.

Naye, Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika cha Maziwa, Mboreny Ulomi, alisema wameamua kuanzisha chama cha ushirika cha maziwa kutokana na kuona maziwa mengi hupotea kwa kuharibika.

Alisema baada ya kuanzisha chama hicho, hivi sasa hakuna maziwa yanayoharibika wala kubaki katika kituo cha kukusanyia.

«Tunawashukuru Kilimanjaro Fresh kwa kuanzisha vituo vya ukusanyaji maziwa kwa kushirikiana na Vyama vya Ushirika vya Maziwa, vinatusaidia kukwepa hasara ya upotevu wa maziwa,»alisema Ulomi.

Alisema kwa sasa wanaendelea kuwasisitiza wafugaji kulisha malisho bora ili waweze kuleta maziwa yaliyo bora katika vituo vya kukusanyia maziwa.

Kwa upande wake, mfugaji na mu[illegible] wa maziwa, Grace Silaha, alisema hiv[illegible] changamoto wanayokumbana nay[illegible] ukosefu wa mbegu bora za ng'ombe am[illegible] wanatoa maziwa mengi.

Kutokana na hilo, Grace ale[illegible] wanaiomba serikali iwasaidie kutafuta mb[illegible] hizo ili waweze kukusanya maziwa m[illegible] kupeleka katika vituo vya kukusanyia ma[illegible]

Grace alisema kwa upande wa s[illegible] la maziwa, lipo hivyo mbegu zikipat[illegible] watapata fursa ya kupeleka maziwa meng[illegible] kuwaingizia kipato cha kutosha.

Alisema bila kufanya hivyo wataen[illegible] kupeleka kiasi kidogo ili hali kiwanda kina[illegible] maziwa mengi kwa ajili ya kutengen[illegible] mnyororo wa thamani.

Scanned with CamScanner



Wahandisi wa umwagiliaji wa mikoa ya Tanzania Bara wakimsikiliza Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo,Gerald Kusaya wakati wa kikao kazi cha Menejimenti ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kilichofanyika Morogoro juzi.(Picha na Wizara ya Kilimo)

HABARI LEO UK 16

‘Ni makosa kuuza ngozi kabla haijawekewa daraja’

Na Lucy Ngowi

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imesema ni makosa kuuza au kununua ngozi kabla haijawekewa madaraja.

Aidha imesema kwa kukiuka utaratibu huo adhabu yake ni faini isiyozidi Sh milioni moja au kwenda jela miezi 12.

Mkurugenzi Msaidizi wa Mazao ya Mifugo, Usalama wa Chakula na Lishe, Gabriel Bura alisema hayo alipokuwa akifungua mafunzo ya waweka madaraja ya ngozi jijini Dar es Salaam.

Bura alisema utekelezaji wa adhabu hiyo unapatikana katika kifungu cha 16 (i) cha sheria ya biashara ya ngozi ambayo ndiyo kiungo muhimu katika uzalishaji wa ngozi bora.

Alisema pia kifungu cha 15 cha sheria hiyo kinaelekeza kuwa mtu yeyote haruhusiwi kuchuna ngozi kwa lengo la biashara, hivyo yampasa awe na leseni ya uchunaji ngozi.

Alisema hadi sasa wizara hiyo imeshatoa mafunzo kwa wachunaji 735 katika mikoa ya Morogoro, Manyara, Arusha, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Kagera, ambapo kati ya hao tayari wizara imeshateua wakaguzi wa ngozi 113 katika wilaya na halmashauri za Tanzania Bara.

Awali alisema kuwa asilimia 10 tu ya ngozi zinazopelekwa kiwandani ndizo zinazofaa kusindikwa huku asilimia 90 zikiwa hazifai kutokana na kukosa ubora unaotakiwa, jambo ambalo limesababisha hasara kubwa kwa wafanyabiashara na wenye viwanda.

Pia alisema Tanzania ni nchi ya pili kwa idadi ya ng’ombe barani Afrika ikiwa na ng’ombe milioni 32.2 baada ya Ethiopia inayokadiriwa kuwa na ngo’ombe milioni 52.

Mifungo mingine iliyopo nchini ni pamoja nan a mbuzi milioni 20, kondoo milioni 5.5 na punda 636,997.

Naye Mteknolojia wa ngozi, Emmanuel Muyinga alisema suala la wizara kuteua wakaguzi wa ngozi ndio ufumbuzi ambao utawafanya wafanye kazi yao kwa kujiamini tofauti na ilivyokuwa awali.

Kwa upande wake Mfanyakazi kutoka kampuni ya ngozi ya ACE iliyopo Morogoro, Godson Shayo alisema mafunzo hayo ya ngozi yamewasaidia kujua ukaguzi wa ngozi ni kitu gani na mhusika anahitajika kufanya nini.

Scanned with CamScanner